NJIA BORA ZA KUDHIBITI UPOTEVU WA NAFAKA BAADA YA MAVUNO

Upotevu wa mazao baada ya mavuno ni nini?

Ni upungufu wa mazao baada ya kuvuna na kabla ya kumfikia mtumiaji. Upotevu unaweza kutokea katika hatua mbalimbali kama vile uvunaji, usafirishaji, uandaaji wa mazao kabla ya kuhifadhi, wakati wa kuhifadhi na uuzaji wa mazao.

HATUA NA AINA ZA UPOTEVU WA NAFAKA

Viwango vya upotevu katika hatua mbalimbali ni kama ilivyo katika kielelezo kifuatacho:



Viwango vya upotevu wa nafaka barani Afrika ni kati ya asilimia 10-23

Aina mbalimbali za upotevu wa mazao

- **Kupungua uzito**- Uzito wa mavuno hupungua wakati wa kuhifadhi ghalani; kwamfano; kwa kupoteza unyevu kupita kiasi, ndege, panya, na viharibifu vingine vinapo shambulia mazao wakati wa kuvuna na kuhifadhi. Pia, kuanguka kwa mavuno wakati wa usafirishaji.
- **Kupoteza ubora**- Njia duni za kuvuna, kuandaa mazao kabla ya kuhifadhi na wakati wa kuhifadhi hupunguza ubora wa mazao. Kwamfano; muonekano wa nafaka, ladha, rangi na harufu.
- **Kupotea kwa virutubisho**- wadudu na panya hushambulia kiini cha punje ambacho kina protini and madini muhimu.
- **Kupotea kwa uhai wa mbegu**- kupoteza hali ya utoaji wa mbegu.
- **Upotevu wa usalama wa mazao**- hutokea wakati viharibifu kama panya na wadudu wengine kushambulia mazao wakati wa kuhifadhi. Pia kuhifadhi mazao yanayozidi kiwango cha unyevu unaoshauriwa kitaalamu na husababisha sumukuvu.
- **Upotevu wa kiuchumi**- Hii hujumisha tafsiri ya upotevu wa malighafi kwa mkulima na ukosefu wa fursa za masoko kwa mazao ya mkulima pia bei duni ya mazao yaliyo haribika na kushambuliwa na wadudu au magonjwa.

Dumuzi

Fukuzi



Kipepeo



Wadudu wengine

Aina za wadudu waharibifu wa mazao ghalani

NJIA NA TEKINOLOJIA ZILIZO BORESHWA ZA KUPUNGUZA AU KUZUIA UPOTEVU WA MAZAO BAADA YA MAVUNO

1. Uvunaji

Visababishi

- Kuchelewa kuvuna na kusababisha uharibifu wa mchwa na punji kudondoka
- Uharibifu wa wadudu, ndege na wanyama

Kinga/ kuzuia

- Vuna kwa wakati kuepuka mazao kushambuliwa na viharibifu vya shambani kama vile mchwa na panya
- Vuna mazao na uhifadhi katika mifuko au vikapu visafi
- Weka mazao yako juu ya turubai baada ya kuvuna toka shambani

2. Usafirishaji toka shambani kuelekea nyumbani

Visababishi

- Punje kudondoka kutokana na mifuko iliyotoboka
- Kuzidisha ujazo katika mifuko na mikokoteni
- Kusafirisha mazao bila kingo za upotevu
- Punje kudondoka katika mifuko ya mikokoteni

Kinga/ kuzuia

- Funika mkokoteni na turubai kabla ya kuweka mazao
- Weka mazao katika mifuko kabla ya kupakia mkokoteni
- Epuka kuzidisha ujazo wa mazao katika mifuko na mikokoteni

3. Ukaushaji

Visababishi

- Kukausha mazao ardhini na maeneo machafu
- Kukausha katika chanja ambayo haijakingwa kuzuia wanyama waharibifu
- Uharibifu wa panya, wadudu, wanyama na wizi
- Unyevu wakati wa kukausha
- Mazao kupungua ubora na kuchangia kuuzwa bei ya chini sokoni

Kinga/ kuzuia

- Epuka kukausha mazao ardhini na maeneo machafu
- Andaa vifaa vya kukaushia kama turubai, mikeka na vinginevyo
- Tumia tekinolojia za kukausha kama kribu, kichanja, au tururubai iliyoboreshwa

Ukaushaji usiofaa

Turubai iliyoboreshwa

4. Kupukuchua

Visababishi

- Kupiga mazao na fito ardhini na katika mifuko
- Punji kuruka mbali na eneo la kupukuchua au kupura
- Punji kuvunjika kutokana na njia ya kupiga fito

Kinga/kuzuia

- Pukuchua au pura mazao kwa kutumia mikono au mashine za kisasa
- Epuka kupukuchua mazao kwa kupiga juu ya ardhi kwa kutumia fito au kwa kukanyaga na trekta

Njia duni au isiyofaa

Njia bora inayofaa

5. Kupepeta

Visababishi

- Njia hafifu zinazotumika kupepeta mazao
- Kupepeta ardhini kwa kutegemea upepo na kusababisha upotevu wa kiasi kikubwa
- Tumia chekeche kutenganisha nafaka bora na uchafu

Kinga/ kuzuia

- Tumia mashine ya kupukuchua ambayo husaidia kupepeta
- Angalia kasi na mwelekeo wa upepo kabla hujaanza kupepeta mazao yako

Njia zisizo faa na njia zilizobora za kupepeta

6. Kuhifadhi

Visababishi

- Mashambulizi ya wadudu, ndege, na panya katika ghala
- Kuhifadhi nafaka pasipo kukauka na kupepetwa vizuri
- Kuhifadhi nafaka katika mifuko na vihenge bila kuchanganya na viuatilifu kwa kuzingatia dozi sahihi
- Kuhifadhi nafaka moja kwa moja sakafuni bila kinga yeyote (kichaja) kuzuia upotevu

Kinga/ kuzuia

- Hifadhi nafaka iliyokauka vizuri na safi
- Tumia viuatilifu sahihi na dozi sahihi vilivyosajiliwa kuchanganya na mazao wakati wa kuhifadhi
- Fuata njia bora za utunzaji wa ghala wakati wa kuhifadhi mazao yako
- Hifadhi mazao katika tekinolojia bora za kisasa m.f mifuko ya PICS, Agroz, au Silo

Aina tofauti za vifaa bora kwa hifadhi ya nafaka bila kemikali vinavyopatikana kwa matumizi ya wakulima wadogo nchini Tanzania

Washirika

Kuhusu Africa RISING

Mpango wa kilimo endelevu Afrika kwa kifupi 'Africa RISING' unajumuisha tafiti tatu za miradi ya maendeleo ambayo inafadhiliwa na shirika la Marekani la Maendeleo ya kimataifa (USAID) kama sehemu ya mpango wa serikali ya Marekani wa kuboresha usalama wa chakula "Feed the Future".

Kupitia utafiti wa vitendo na ushirika wa maendeleo unaofanywa na Afrika RISING, umepelekea kujenga fursa kwa wakulima wa kaya maskini kuondokana na umaskini, kupitia mfumo wa kilimo endelevu. Mfumo huo unaboresha chakula, lishe na usalama wa mapato, haswa kwa wanawake na watoto; na kuhifadhi au kuongeza msingi wa rasilimali asilia.

Miradi mitatu inaongozwa na Taasisi ya Kimataifa ya kilimo kwenye ukanda wa Tropiki (Magharibi, Mashariki na Kusini Afrika) na Taasisi ya utafiti wa mifugo ya Kimataifa (katika nyanda za juu za Ethiopia). Taasisi ya kimataifa ya Sera ya chakula inahusika sambamba kuongoza mradi katika kufuatilia na kutathimini maendeleo ya mradi na athari zake.